UQAB
Jarida la

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Bei ghali ya Mafuta: Kufeli Kiujumla Kwa Mfumo wa Ubepari wa Kiushuru

**HABARI NA MAONI**
Kuhifadhi Utumwa wa Kikoloni ili Kupata Malipo Duni

**TOLEO JIPYA**
Serikali Mpya Nchini Afghanistan

**JIBU LA SWALI**
Namna ya Kuamiliana na Ukaaji Uchi Ulioenea



Afisi ya Habari
ya Hizb ut Tahrir
Kenya

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ مِنكُمْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي ٱلْأَرْضِ كَمَا ٱسْتَخْلَفَ ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ ٱلَّذِي ٱرْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْـًٔا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْفَٰسِقُونَ﴾

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 03/1443 | Jumatano, 08 Safar 1443 H | 15/09/2021 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Bei ghali ya Mafuta:Kufeli Kiujumla Kwa Mfumo wa Ubepari wa Kiushuru

Kama ilivyotarajiwa, kwa mara nyengine tena bei ya mafuta imepanda maradufu kuwahi kushuhudiwa katika historia ya Kenya baada ya serikali kusitisha mpango wake wa kulipia gharama za bidhaa za petroli ulioanzishwa mwezi Aprili mwaka huu kama njia ya kuepusha hasira za raia dhidi ya gharama kubwa za maisha. Mamkala ya Kudhibiti Kawi na mafuta EPRA iliondosha mapungufu ya bei ya mafuta yaliyouzwa katika mwezi uliopita hadi Septemba 14;Ksh 7.10 kwa petrol, Ksh 9.90 kwa Dizeli na kwa mafuta Ksh 11.36. Jijini Nairobi lita moja ya petrol sasa ni Ksh 134.72 baada ya bei ya awali ya Ksh 127.14. Bei ya Dizeli iliokuwa Ksh 107.66 sasa imepanda hadi Ksh.115.60 na mafuta ya taa sasa yakiuzwa kwa Ksh.110.82 kutoka kwa Ksh.97.85 hapo awali.

Kinachotamausha, ni kwamba kupanda huku kwa bei kunakuja wakati ambapo maeneo ya kaskazini na pwani ya nchi yanakodolewa na baa la nja kutokamana na ukame uliotangazwa kuwa ni janga la kitaifa. Gharama ya juu ya mafuta huathiri pakubwa karibu sekta zote za uchumi na huwa na athari kubwa gharama za maisha. Hii ni dhahiri shahiri kwamba mataifa ya kibepari huzidishia raia wake maumivu zaidi na viongozi wake hawajali kikweli maslahi ya raia wanaodai kuwaongoza.

Kuhusu suala la kupanda kwa bei ya mafuta, hii husababishwa na mambo mawili nayo: ukiritimba katika uzalishwaji wa rasilimali hii na suala la utozwaji ushuru katika viwanda vya kawi. Kimataifa, maeneo yanayozalisha mafuta yanamilikiwa na makampuni makubwa ya Kimagharibi ndani ya mwavuli wa shirika la nchi zinazosafirisha mafuta duniani (OPEC). Ukiritimba wa mali hii yenye thamani kubwa ya kiuchumi kumefanya mataifa ya ulimwengu wa tatu uwe chini ya matakwa ya OPEC kwenye suala la uzalishaji wa mafuta, usambazwaji wake na hata bei. Mabepari ndio hutumia OPEC kama zana ya kudhibiti na kupelekea masuala yote ya biashara ya mafuta. Uhalisia huu kikamakusudi huwa hauzungumziwi bali hupuuzwa na Warasilimali wa Kimagharibi. Ama kuhusu utozaji ushuru hili liko bayana kwani serikali huweka ushuru mwingi katika bidhaa za mafuta. Muhimu kubainika kwamba katika mfumo wa Kirasilimali njia rahisi ya serikali kupata mapato yake ni kupitia kutosha ushuru wa mafuta. Kwa hali yetu hapa Kenya kwa mfano hukusanya jumla ya shilingi 57 za ushuru wa Petroli, Shilingi 45.47 kwa Dizeli na shilling 39.5 kwa mafuta ya taa. Ongezeko hili la bei ni jaribio jengine la serikali kuokoa uchumi wake unaoendelea kudorora huku ikiwa mfumuko wa bei ukiwa asilimia 6.6 dhidi ya dollar. Kuanguka kwa thamani ya shilingi ni dalili wazi ya kusuasua kwa hali ya uchumi hasa ikizingatiwa uchumi wa Kenya unategemea uagizaji mno wa bidhaa na kufanya kuweko mwanya mkubwa baina ya bidhaa zinazoagizwa kutoka nje na zile zinazosafarishwa nje kwa shilingi hali inayofanya serikali iweze kutoza bidhaa za mafuta. Yasikitisha tukitabiri kwa hali hii tata ya kiuchumi huenda ikapelekea marufuku ya uagizwaji wa bidhaa zisizokua na umuhimu kama njia ya kujaribu kunasua mdororo wa shilingi na uchumi dhidi ya makali ya Dollar.

Kwa hali hii tulioangazia,ni wazi kwamba utawala wowote unaopeleka mfumo wake kwa misingi ya mikopo ya uchapishaji pesa za makaratasi ni wenye kusababishia maafa zaidi kwa raia wake. Isitoshe, uchumi nchi yoyote leo umefungwa na matakwa na maoni ya serikali kuu duniani – Marekani. Ongezeko la bei ya mafuta na tatizo lolote la kiuchumi litatatuliwa tu na Dola ilio huru kikweli inayotekeleza Mfumo wa Kiuchumi wa Kiislamu uliobaini kwamba mali kama vile Maji, Malisho na Kawi yote haya ni mali ya umma kama ilivyosimuliwa na Ibn Majah kwamba Mtume SAAW alisema:

«الْمُسْلِمُونَ شُرَكَاءُ فِي ثَلَاثٍ: فِي الْمَاءِ وَالْكَلَإِ وَالنَّارِ»

**“Waislamu wana ushirika kwa mambo matatu: Katika Maji, Malisho na Kawi.**

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Hizb ut Tahrir Kenya**

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Sera ya Vyombo vya Habari ya Khilafah Pekee Ndio Inayohakikisha Uwajibikaji Huku Vyombo vya Habari Vikiwa ni Ala Yenye Nguvu ya Kubeba Ukweli wa Uislamu Ulimwenguni

Wanahabari, vyombo vya habari, mawakili, vyama vya upinzani na mashirika ya kutetea haki za binadamu ya Pakistan wanapambana na Mswada wa Maendeleo ya Vyombo vya Habari wa Pakistan, wakiulaani kama jaribio la kuvinyonga vyombo vya habari. Kwa upande mwingine, serikali inadai haja ya kuzuia habari bandia na kutoa haki kwa wafanyikazi wa vyombo vya habari. Huku wakiwa na huruma chache kwa upinzani, Waislamu pia wanaona kuwa serikali inanyonga kila aina ya uwajibikaji, ikiwemo utekaji nyara wa hivi karibuni wa wanaharakati sita wa Hizb ut Tahrir kutoka Karachi, kwa sababu tu ya kufichua msimamo unaoegemea upande wa Amerika wa serikali kwa Afghanistan.

Vile vile, serikali huwateka nyara waandishi wa habari, ikiwashinikiza kueneza hadithi ya serikali. Ummah inaona kuwa sehemu kubwa ya vyombo vya habari vimekuwa chombo cha ukoloni, katika kuhudumia serikali au dola za kigeni, vikipotosha Ummah kupitia hadithi huria, zenye kupinga Uislamu. Kwa hivyo, vyombo vikuu vya habari vimepoteza uaminifu, huku Ummah ukielekea kwa vyombo vya habari visivyo vya kawaida, kama mtazamaji asiyevutiwa na mgogoro ulioko sasa.

Vyombo vya habari ni tawi la kudumu la serikali katika dola ya Khilafah, huku vyombo vya habari mahiri vya kibinafsi vitashajiishwa. Vyombo vya habari ni sehemu isiyoweza kutenganishwa ya sera ya dola ya kuutawalisha mfumo wa Kiislamu kote ulimwenguni. Hakuna leseni inayohitajika kwa aina yoyote ya chombo cha habari, ikiwa inatosha tu kwake kuifahamisha dola kubuniwa kwake pekee. Kila chombo cha habari kinawajibika kwa habari zake zilizochapishwa au zilizoripotiwa, kuhisabiwa mbele ya mfumo huru wa mahakama ya Kiislamu ikiwa kutakiukwa sera ya vyombo vya habari. Msingi wa uwajibikaji wa dola ni sera ya Kiislamu ya kuamrisha mema na kukataza maovu, sio uhuru wa kujieleza, kutoka kwa ustaarabu wa kiliberali wa Magharibi. Hakuna chombo chochote cha habari kitakachopewa idhini kuanzisha uhusiano huru na serikali au taasisi za kigeni.

Vyombo vya habari haviwezi kutoa vyenzo zisizo za Kiislamu wala kuhujumu msingi wa dola, kwani Waislamu wote na waandishi wa habari wana haki ya kikatiba ya kuwawajibisha watawala na maafisa wa serikali kwa msingi wa Uislamu, kama vile Mwarabu mmoja Mbedui alivyomuuliza Umar (ra) kuhusu shuka mbili alizokuwa anazimiliki, au mwanamke mmoja kumlazimisha Umar (ra) kubadilisha amri yake juu ya mahari. Kila chombo cha habari kinawajibika kwa habari zake zilizochapishwa au zilizoripotiwa, chenye kuhesabiwa mbele ya mfumo huru wa mahakama ya Kiislamu.

Katika demokrasia na udikteta, sheria ni kwa kufuata matakwa ya wanadamu, badala ya kuvuliwa kutoka kwa Quran na Sunnah. Kwa hivyo watawala wanazuia vyombo vya habari ili kulinda maslahi ya kibinafsi na ya wakoloni, huku baadhi ya vyombo vya habari vyenye nguvu vikifanya vivyo hivyo. Vyombo vya habari vya Khilafah ndivyo vitakavyofanya kazi chini ya sera isiyoweza kubadilishwa ya Shariah ya Kiislamu, ambayo haiwezi kuharibiwa na Khaleefah wala Baraza la Ummah. Vyombo vya habari hivyo vitazindua kampeni ya kiulimwengu dhidi ya dola za kirasilimali, vikifichua sera zao angamivu za kikoloni na itikadi na mifumo batili, vikiandaa uwanja wa ufunguzi wa Uislamu wa ardhi zao. Baada ya kuzipata nyoyo na akili za watu wao kwa uadilifu wa Uislamu, jeshi litatumwa kuwaondoa watawala wanaobakia kama kizingiti. Na ni vyombo vya habari kama hivyo vya Kiislamu ambavyo vitamhisabu mtawala awajibike, bila kumuogopa yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu (swt), kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (swt). Hivi vitakuwa ni vyombo vya habari vinavyoweka mifano katika ushujaa, ukweli na unyofu.

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah Pakistan**


Email: info@uqab.or.ke

# Ripoti ya Kadhia ya Hamza si ya Kuaminika, na Inadhihirisha Uwongo katika Kesi za Ugaidi Tanzania



**Habari:**

Mnamo tarehe 2 Septemba, 2021 Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) nchini Tanzania Bw. Camilius Wambura alitoa ripoti yake kuwa Hamza Mohamed (30) mfanyabiashara na mwanachama wa chama tawala (CCM) aliyeuawa na polisi siku ya tarehe 25 Agosti 2021 baada ya kuwaua askari watatu na mlinzi mmoja jijini Dar es Salaam kwamba alikuwa gaidi wa kujitoa muhanga.

**Maoni:**

Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai bwana Wambura alidokeza kuwa uchunguzi wake zaidi ulijikita katika maeneo matatu: ambayo ni kufahamu utambulisho wa Hamza Mohamed, kilichompelekea kufanya mauaji, na ni kina nani anaoshirikiana nao.

Kuhusiana na utambulisho wa Hamza, uchunguzi umedai kubaini kuwa alikuwa akiishi maisha ya siri yaliyokuwa na viashiria vya ugaidi aliojifunza kupitia mitandaoni.

Kuhusu kilichompelekea kufanya mauaji yale, uchunguzi umeweka wazi kuwa alikuwa gaidi mwenye msimamo mkali wa kidini aliyekuwa tayari kuifia dini yake.

Ama ni kina nani anaoshirikiana nao, uchunguzi umeeleza kuwa Hamza alikuwa ana mawasiliana ya moja kwa moja na watu katika nchi zenye uwezekano na mafungamano na ugaidi, japo inafahamika wazi kuwa, watu watano bado wanashikiliwa na polisi kuhusu suala hili.

Ripoti hii ya uchunguzi ni finyu, iliyokosa weledi na iliyoegemea upande mmoja, kwani taarifa zake zinapingana na uhalisia. Takriban watu wote waliohojiwa na vyombo vya habari kuhusu Hamza, Waislamu na wasiokuwa Waislamu, ndugu, marafiki, wanachama wenzake, wafanyakazi wake, majirani nk walikuwa na jibu moja tu na mtazamo chanya kuwa Hamza alikuwa mtu mwema mwenye maadili mema ya dini ya Kiislamu. Venance Kalinga, jirani wa Hamza alinukuliwa akisema kuwa Hamza “ni mtu mwenye maadili anayefuata mafundisho ya Kiislamu, anapenda kwenda msikitini kila asubuhi, mchana na jioni” (Reuters 02/09/2021). Zaidi ya hayo yote Hamza alikuwa mfanyabiashara akijumuika na watu ikiwemo kuajiri wafanyakazi. Hivyo, maisha ya Hamza hayakuwa ya usirisiri na yasiyofahamika kama ilivyoripotiwa bali alifahamika na watu wengi waliotokea kuishi naye.

Dhana kwamba Hamza alijifunza ugaidi kupitia mtandao wa internet na mitandao ya kijamii haina msingi wowote na ni hoja iliyokosa uwazi, kwani ripoti imeshindwa kabisa kutaja ukurasa, tovuti au mitandao ipi ya kijamii aliyoitumia. Kiukweli nukta hii inaibua maswali mengi kuliko majibu, kwa mfano, vipi mtu anaweza kujifunza kwa mtandao kutungua kwa bunduki, na vipi angeweza kufanyia mazoezi ulengaji shabaha kupitia mitandao? Na kama walilifahamu hilo, kwa nini hawakumzuiya? Kama Hamza alikuwa na viashiria vya ugaidi, vipi aliweza kuwa mwanachama mashuhuri wa chama tawala (CCM), bila ya kutaja kumiliki kwake silaha kisheria? Haya yote yanaonesha ripoti ni batili na haina uhalisia.

*Endelea... UK 5*



Email: info@uqab.or.ke

Kuhusiana na suala la kuwa eti msimamo mkali wa dini wa Hamza ndio uliomshawishi kufanya mauaji, hili pia halikinaishi, bali kimsingi limetumika kutusi dini ya Hamza ambayo ni Uislamu. Ni jambo lenye kufahamika wazi kuwa Uislamu hauruhusu mauaji ya watu wasio na hatia. Hivyo, ripoti hii ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai ni jaribio la kuuchafua Uislamu na kamwe halikubaliki. Kiuhalisia ripoti imeshindwa kuonesha uhusiano kati ya dini ya Hamza na kile ilichokiita ugaidi. Hii inaonesha kuwa kujaribu kuunganisha baina ya dini ya Hamza na mauaji ya polisi ni jambo lisilo na msingi wowote.

Maelezo ya ripoti kuwa Hamza alikuwa na mawasiliano na watu katika nchi zenye uwezekano wa kuwa na ugaidi, kwa mara nyengine imeshindwa kutaja nchi mahsusi na watu hao. Hata hivyo, kwa jinsi propaganda chafu za vita dhidi ya ugaidi zilivyo duniani, suala la ugaidi lipo kila nchi. Je hili ndio limemtosha Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai kuthibitisha madai ya ugaidi dhidi ya Hamza?

Ugaidi kama maarufu unavyotafsiriwa kimataifa kama matumizi yasio halali ya nguvu dhidi ya raia kufikia malengo fulani ya kisiasa. Kwa muktadha wa Hamza, ripoti imeshindwa kuelezea ni malengo gani ya kisiasa aliyotaka kuyafikia. Kinyume chake, kwa vile Hamza alikuwa mwanachama wa chama tawala (CCM) ni wazi kuwa alitumia njia ya kidemokrasia kufikia malengo yake ya kisiasa. Hili linatilia mkazo mtazamo wa wengi kuwa tukio hili la mauwaji halikuwa la ugaidi bali uhalifu wa kawaida.

Pia ripoti ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) inaonesha kukosa uaminifu kwa vile imepuuza maneno ya Hamza kabla ya kuuawa na Polisi tarehe 25 Agosti mwaka 2021 ambapo alitoa madai yake dhidi ya polisi hususan Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) Simon Sirro kwa kuhusika kwao katika kuuwa Waislamu. Suala la ukatili wa polisi, mauwaji, mateso, kunyakua, kudhalilisha Waislamu wasio na hatia nchini Tanzania linafahamika shahir dhahir, na hii ni mifano michache:

Mnamo tarehe 14/01/2006, Juma Ndugu, Muislamu, dereva wa teksi na wafanyabiashara watatu wa madini kutoka Mahenge mkoani Morogoro waliuawa kikatili katika msitu wa Pande, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam na aliyekuwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Wilaya ya Kinondoni (SP) Christopher Bageni. (Global Publisher 16/09/2016)

Kadhalika, mwezi Mei mwaka 2017, askari Polisi walimuua Salum Muhammad Almas aliyekuwa Imamu na mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika eneo la Kurasini jijini Dar es Salaam kwa kumtuhumu tu na uporaji bila ya kuwa na ushahidi wowote.

Aidha, tarehe 21/07/2017, Polisi walivamia Waislamu wakiwa katika ibada katika Msikiti wa Ali Mchumo katika wilaya ya Kilwa na kuteka Waislamu 10. Baadaye baadhi waliripotiwa kufariki dunia na baadhi kupata ulemavu kutokana na mateso waliyopewa na Polisi. (Mwananchi 27/07/2017 & Mwananchi Digital 09/04/2018)

Kwa kuongeza, ikumbukwe kuwa ripoti ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai ilinajisiwa awali kwa kuwa ilitanguliwa na msimamo wa IGP kuwa Hamza alikuwa na uhusiano na wapiganaji wa Msumbiji, na kuwa shambulizi lake linaweza kuhusika na ushiriki wa Tanzania katika mapigano nchini Msumbiji. Kauli hii ndio iliyochora sura ya matokeo ya uchunguzi wa ripoti ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai.

Kwa kukhitimisha, ripoti ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai sio tu imejifedhehi wazi wazi kuwa iliegemea upande mmoja, bali pia imethibitisha uwongo juu ya kutokamilika kwa upelelezi dhidi ya Waislamu wanaotuhumiwa kwa makosa ya ugaidi.

Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai ameweza ndani ya wiki moja kufanya upelelezi na kugundua kuwa Hamza alikuwa gaidi licha ya mtuhumiwa kutokuwepo, ilhali kuna mamia ya Waislamu wametuhimiwa kwa makosa ya ugaidi katika mikoa mingi nchini ikiwemo Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya, Tanga na Mtwara ambako wanaharakati watatu wa Hizb ut Tahrir Tanzania; Ustadh Ramadhan Moshi Kakoso, Omar Salum Bumbo, na Waziri Omari Mkaliaganda wanashikiliwa kwa miaka minne sasa kwa makosa ya kubambikiwa ya ugaidi kwa kisingizio cha “upelelezi kutokamilika”.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Said Bitomwa**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania**

# HABARI NA MAONI
# Kuhifadhi Utumwa wa Kikoloni ili Kupata Malipo Duni

**Habari:**

Base Titanium, kampuni ya kuchimba madini katika Kaunti ya Kwale, ililipa kampuni iliyo na mahusiano nayo ya Base Resources kitita cha bilioni Sh6.5 katika mwaka uliioisha Juni, ikiashiria faida kubwa katika biashara yake ya uchimbaji madini. Malipo hayo yaliiweka kampuni hiyo kuwa nambari mbili katika orodha ya kampunii ya kigeni ambayo migao yao imewekwa wazi. South Africa Vodacom Group ndio ya kwanza yenye kupata mgao mkubwa kutoka soko la nchi, ikipokea pato la bilioni Sh19.2 kutoka kwa Safaricom kwa mwaka ulioisha Machi. (Business Daily, Alhamisi 09/09/2021).

**Maoni:**

Kenya kama shamba la kikoloni la Uingereza, sera zake zimetiwa minyororo zikizingatia maslahi ya bwana. Maslahi ambayo msingi wake ni nidhamu ya kiuchumi ya kirasilimali ya kisekula. Hivyo basi natija yenye hatari lazima ienee kote katika shamba la kikoloni! Maslahi ya bwana yanaweka kipaumbele yafuatayo:

**Kwanza,** kuwaweka watawala vibaraka watiifu wasiona mbali, wenye kupiga hesabu za muda mfupi na kumakinisha kipote kichache wa wanasiasa watiifu.

**Pili,** kuwadhoofisha raia wenyeji kupitia mipango ya kuwatoza ushuru wenye kuwakandamiza amali zao za kiuchumi ili kuhakikisha kuwa hawawi tishio kwa kipote kilichomakinika.

**Tatu,** kuulinda uwekezaji wa kampunii ya kigeni kwa kutumia kila mbinu hata ikibidi kuvunja sheria na kanuni zozote kwa kisingizio cha kinga kwa miradi ya uwekezaji wa kigeni wa moja kwa moja.

**Nne,** kuripoti kwa uchache rasilimali zilizopo na utoaji wa mikataba ukiwa umezingirwa na usiri huku kukikosekana uwajibikaji.

**Tano,** kuendelea kuisifu sura ya bwana nchini na kimataifa ili kuhakikisha ukiritimba wake unakita shambani! Kupitia kutekeleza mfumo wake wa kirasilimali wa kisekula na nidhamu zake zilizo na sumu kama vile nidhamu ya elimu ya kisekula, nidhamu ya kiuchumi ya kirasilimali, nidhamu ya kijamii huria na nidhamu ya utawala ya kidemokrasia n.k.

Hayo hapo juu ni baadhi ya misingi ambayo inachora njia zenye kufuatwa na tawala sio tu nchini Kenya bali duniani kote ambako Uingereza na washirika wake wana ushawishi. Hivyo basi, sio jambo la kushangaza kushuhudia ripoti za kutamausha za malipo makubwa kwa kampunii ya kigeni ambayo yanapora rasilimali za nchi kwa uchu na kiu chao kisichoisha! Kwa kuongezea, serikali zimeridhika na vijiada vinavyolipwa na kampunii hayo.

Kwa hakika, hiyo ndio bei ambayo mataifa hulipa kwa ajili ya kuhifadhi utumwa wao wa kikoloni kwa mabwana zao Wamagharibi. Pasina kuzingatia madhara yasiyohesabika yanayopatikana kupitia mahusiano hayo.

Kinyume chake ni nidhamu ya utawala ya Kiislamu, Khilafah iliyosimamishwa tena kwa njia ya Utume, inaelekeza kwamba Khilafah ni mlinzi na ngao kwa raia wake. Ipo kwa ajili ya kusitisha ufujaji wa rasilimali za umma na dola kupitia kampuni za kigeni au watu binafsi huku raia wakihangaika! Badala yake Khilafah itajizatiti kutumia rasilimali kwa manufaa ya raia kama ilivyopangiliwa katika nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu iliyotolewa kutoka vyanzo vya Kiislamu vya Shari'ah (Qur'an, Sunnah, Ijm'a Sahaba na Qiyas).

Kwa kuongezea, Khilafah sio zana ya kikoloni inayotegemea michoro ya kikoloni. Kwa sababu hiyo itafanya hima kubakia huru kutokamana na wakoloni Wamagharibi kwa kufichua mfumo wao wa kirasilimali wa kisekula na nidhamu zake ovu ambazo ndio chanzo cha majanga yanayoikumba dunia leo. Kwa hivyo, Khilafah itakwenda mbio kutatua tatizo la kweli la kiuchumi ambalo ni usambazaji wa rasilimali kwa raia ili waweze kukidhi mahitaji yao msingi: chakula, mavazi na makazi. Pia mahitaji ya kijamii: elimu, usalama na huduma ya afya; na mahitaji ya ziada. Ikilinganishwa na nidhamu ya kiuchumi ya kirasilimali ni kinyume. Kwani inadai kuwa tatizo la kiuchumi ni uhaba wa rasilimali. Kwa hiyo ipo kuzidhibiti rasilimali ziwafae wachache wenye ushawishi kwa gharama ya maskini!

**Imeandikwa kwa ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Serikali Mpya Nchini Afghanistan

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Adnan Khan**

Taliban hivi karibuni imetangaza serikali mpya ya mpito baada ya mabatilisho na ucheleweshaji wa mara kadhaa. Dunia imekuwa ikiiangalia Afghanistan kwa karibu zaidi tokea Taliban wauondoe utawala ulioungwa mkono na Amerika jijini Kabul. Taliban imekuwa ikifanya mikutano na mataifa ya kieneo na viongozi wa idara za kijasusi. Kwa kutekwa mkoa wa Panjshir na kushindwa kwa Natinal Resistance Front (NRF), Taliban hatimaye imejihakikishia kutangaza serikali yake mpya ya mpito.

Walinzi wa zamani wa Taliban wameihodhi serikali mpya licha ya ahadi ya kuweka serikali shirikishi. Kati ya wahusika 33 waliotangazwa, 14 ni maafisa wa zamani wa Taliban wa wakati wa utawala uliopita 1996-2001, watano ni wafungwa wa zamani wa Guantanamo na waliobaki 12 ni maafisa kutoka kizazi cha pili cha harakati hiyo. Baraza lote la wanaume litaongozwa na Mullah Muhammad Hassan Akhund, mmoja ya waasisi wa harakati na naibu Waziri Mkuu na waziri wa mambo ya nje wa wakati wa kipindi cha miaka mitano ya kujinyima ya Taliban ilipokuwa ikitawala. Akhund yupo kwenye vikwazo vya UN kutokana na jukumu lake katika kipindi hicho. Sirajuddin Haqqani, aliye katika orodha ya wanaosakwa na FBI ataongoza wizara ya mambo ya ndani. Mtandao wa Haqqani ulikuwa nyuma ya baadhi ya mashambulizi mabaya zaidi dhidi ya Amerika na vikosi vya washirika wakati wa vita vya miaka 20.

Mtoto wa muasisi wa Taliban Mullah Omar, aitwaye Mullah Yaquub, atakuwa waziri wa ulinzi, na waziri wa mambo ya kigeni atakuwa Amir Khan Muttaqi ambaye ni kiongozi wa ngazi ya juu. Mullah Abdul Ghani Baradar, mmoja wa washiriki waazilishi, atakuwa mmoja ya wasaidizi wawili wa Waziri Mkuu. Baradar mwanzoni alikuwa kiongozi wa afisi ya kisiasa ya Taliban, iliyopo Doha na alisimamia utiaji saini wa mkataba wa amani na Amerika mwaka jana. Baradar alitolewa gerezani mnamo 2018, baada ya kutumikia kwa miaka minane, ikiwa ni sehemu ya mpango wa kufanikisha Mchakato wa Amani. Mnamo 2020, Baradar akawa kiongozi wa mwanzo wa Taliban kuwa na mawasiliano ya moja kwa moja na raisi wa Amerika baada ya kuwa na mawasiliano na Donald Trump.

Taliban inajikuta ikikabiliana na changamoto nyingi hivi sasa inapounda serikali. Wanahitaji kuvuka kutoka katika harakati ya msituni kuelekea kwenye serikali. Taliban inahitajia hivi sasa kutoa huduma za serikali, kuhudumia miundo mbinu na kuzalisha uwekezaji wa umma kusaidia ukuaji katika uchumi wa Afghanistan unaotegemea misaada kwa kiasi kikubwa. Kwa mujibu wa ripoti ya Februari ya 2021 iliotolewa na Kundi la Uchunguzi la Afghan la serikali ya Amerika, kiwango cha umasikini nchini Afghanistan hivi sasa kinakisiwa kuwa ni zaidi ya asilimia 72, kutoka asilimia 55 mwaka 2017.

Taliban itahitaji msaada wa maafisa wa utawala wa zamani, angalau kwa viwango vya chini, kuhakikisha uendeshaji mzuri wa usimamizi wa mambo ya kila siku. Hili bado halijatekelezwa licha ya mkono mrefu wa Taliban. Maafisa waliotumikia utawala wa Ghani wametakiwa kurejea Afghanistan na Waziri Mkuu Akhund wa Taliban akiahidi “itahakikisha usalama na amani yao.” Pia shirika la Amnesty limeahidiwa (usalama) kwa kila aliyefanya kazi pamoja na Amerika na idara zilizopita zilizoungwa mkono na Amerika baada ya uvamizi wa 2001.

Taliban imeelezea hamu yake ya kutambuliwa kimataifa na kuanzisha mahusiano ya kidiplomasia ikielezea kuwa wanataka “mahusiano imara na mazuri pamoja na majirani zetu na nchi nyengine zote yakizingatia kuheshimiana na maingiliano” wakiongezea kuwa wataheshimu sheria na mikataba ya kimataifa “ambazo hazigongani na sheria za Kiislamu na maadili ya kitaifa ya nchi .”[4] Jamii ya kimataifa, kwa upande mwengine, maingiliano baina yao yamekuwa ya polepole. Taliban imeiweka China kuwa ni mshirika muhimu katika eneo. Kwa kuzingatia haya, China imetangaza kutoa dolari milioni 31 za misaada ya dharura inayojumuisha nafaka, mahitaji ya kipindi cha baridi pamoja na dozi milioni tatu za chanjo ya Covid-19.

Hakukuwa na taarifa zinazohusiana na sera na vipaumbele vya serikali mpya ya mpito hasa ikizingatiwa ukweli kuwa nchi hiyo inategemea misaada ya kigeni. Licha ya kutangaza serikali yake mpya, Taliban inakabiliwa na changamoto lukuki.

**#أفغانستان** **#Afganistan** **#Afghanistan**

# Usalama wa Wanawake ni Sarabi Ndani ya Mji Mkuu wa India ya Kiliberali



Hasira za watu zinaongezeka siku hadi siku kutokana na mauaji ya Sabiya Saifi aliyejitolea kwa ajili ya Ulinzi wa Raia. Madai ya haki kwa Sabiya yanaongezeka sio tu jijini Delhi, bali hadi UP [Uttar Pradesh], Uttarakhand, Bihar, Maharashtra na majimbo mengine ambapo maandamano ya mishumaa yanafanyika. [Gazeti la Siasat daily, 7 Septemba 2021]

Tukio hili la kuumiza moyo la mauaji ya kikatili ya msichana mdogo wa Kiislamu kwa kuchomwa visu karibia mara 50; titi lake kukatwa pamoja na vidonda kadhaa mwili mzima ikiwa ni pamoja na sehemu za siri na kutupwa kwenye vichaka jijini Delhi ilisababisha wimbi la mshituko kote nchini, vyombo vingi vya habari vilishindwa kutangaza taarifa yoyote kuhusu mauaji haya ya kikatili. Isipokuwa baada ya kuvuma kwa hashtagi katika akaunti za mitandao ya kijamii kwa muda wa wiki isemayo #JusticeForRabia (haki kwa Rabia), vyombo vya habari vichache vilichapisha habari kuhusiana na suala hili. Ni wazi kabisa inaonyesha majadiliano ya kudhibiti tukio hili yanayofanywa na mashirika ya habari ya kitaifa yanayofanya kazi ndani ya nchi kubwa ya kidemokrasia duniani. Wazazi na kaka wa marehemu walisema walikabiliwa na changamoto kadhaa na ugumu kabla ya kuweza kufungua faili la malalamiko. Kumekuwa na maandamano machache yanayodai uchunguzi ufanywe na CHOMBO KIKUU CHA UPELELEZI, huku polisi wa Delhi wakijaribu kuifunga kesi kwa maneno ya uwongo. Hii inaonyesha kiwango cha ufisadi ndani ya idara ya usalama na thamani iliyotolewa kwa usalama wa wanawake ndani ya nchi yao wenyewe. Hata hivyo, vyombo vya habari vya ndani vilivyozoeleka vilikuwa na wasiwasi sana kuhusu siku zijazo juu ya haki za wanawake na usalama wao nchini Afghanistan baada ya Taliban kuichukua Kabul. Ni wazi matukio haya yanaonyesha unafiki wa vyombo vya habari juu ya uhalisi wa kweli wa usalama wa wanawake na 'uwezeshaji' ndani ya nchi kubwa ya kidemokrasia duniani ambayo inaunga mkono uhuru wa Kimagharibi.

Hii sio mara ya kwanza uhalifu wa aina hii dhidi ya wanawake kuripotiwa nchini India; matukio kadhaa kama kesi ya ubakaji ya Nirbhaya (2012), kesi ya ubakaji ya Unnao (2017), kesi ya ubakaji ya Kathaua (2018) na kesi ya ubakaji na mauaji ya Hyderabad (2019) yanafichua uhalisia mbaya wa uhalifu wa kinyama wa kijinsia dhidi ya wanawake nchini. Utafiti uliofanywa na Taasisi ya Thomas Reuters mwaka 2018 uliiweka India kama nchi hatari zaidi kwa wanawake. Kwa mujibu wa Afisi ya Kumbukumbu za Uhalifu wa Kitaifa (NCRB), India ilirekodi kesi za ubakaji 88 kila siku ndani ya mwaka 2019. Ripoti ya NCRB inaonyesha kuwa mazingira makubwa ya ubakaji wa msichana au mwanamke yameongezeka kufikia asilimia 44 kwa miaka 10 iliyopita. Kuhusu Delhi, sio tu ni mji mkuu wa kisiasa lakini pia ni mji mkuu wa ubakaji ambao unarekodi ya idadi kubwa zaidi za ubakaji kuliko miji mingine nchini India; Katikati ya Januari 1 na 15 Juni 2021, polisi wa mji huo walisajili kesi 833 za ubakaji na 1,022 za unyanyasaji, juu zaidi kutoka kesi 580 za ubakaji na 735 za unyanyasaji

*Endelea... UK 9*

zilizofunguliwa ndani ya kipindi kama hicho mwaka uliopita.

Tokea kuvunjwa kwa Khilafah, ulimwengu umekosa utawala wa marejeo, jamii ya marejeo, mfumo wa marejeo kwa wanadamu; Kila mfumo uliotengenezwa na mwanadamu umekuwa ukiwakandamiza wanadamu na wanawake ndani ya jamii zao; watu weusi wanaonewa kidhati ndani ya mataifa ya Magharibi; uwonevu kwa Waislamu wa Uyghur ni sera maalumu iliyowekwa na China; vivyo hivyo, kuna mfumo maalum wa kugawa jamii ya India, ambapo kama mwathirika ni Muislamu au ni wa jamii ya Dalit [tabaka duni la kibaniani], basi vyombo vya habari havitachukulia uzito na muda mwengine wanashindwa kutangaza habari hio kwa ulimwengu, na taasisi za serikali fisidifu zinashindwa kuwaadhibu wahusika kwa mwenendo kama huo. Hata hivyo, kama mwathirika ni wa ‘tabaka la juu’ la jamii hiyo, hapo ndipo vyombo vya habari, polisi na mahakama vinafanya kazi kwa haraka mpaka uamuzi unapitishwa na mhalifu anaadhibiwa.

Dunia haitoweza kufikiria kuhusu jamii yoyote ambayo ilikuwa ni ya mfano katika kusimamisha haki isipokuwa jamii ya Kiislamu. Mfumo wake wa utawala ulisimamisha haki kati ya matabaka ya watu tofauti tofauti kwa kutekeleza Sheria na kuadhibu wahusika wa uhalifu bila ya kujali dini, rangi au kabila. Msingi wake wa kiroho wa kujisalimisha kwa Muumba uliifanya jamii hii iwe ya tofauti na ya kushangaza kuliko ustaarabu wowote katika historia ya binadamu.

Amri ya Mungu ya kusimama imara kwenye upande wa haki imewekwa wazi katika aya ya Qur’an ambapo Mwenyezi Mungu (SWT) asema;

(يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُونُوا قَوَّامِينَ لِلَّهِ شُهَدَاءَ بِالْقِسْطِ وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَآنُ قَوْمٍ
عَلَى أَلَّا تَعْدِلُوا اعْدِلُوا هُوَ أَقْرَبُ لِلتَّقْوَى وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ)

**"Enyi mlio amini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mkitoa ushahidi kwa haki. Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamngu. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda"** [Surat Al-Maida: 8]

Hili pia limesisitizwa katika Sunnah ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) kama ilivyoripotiwa katika Bukhari. Mtume (saw) amesema:

«إِنَّ بَنِي إِسْرَائِيلَ كَانَ إِذَا سَرَقَ فِيهِمُ الشَّرِيفُ تَرَكُوهُ، وَإِذَا سَرَقَ الضَّعِيفُ
قَطَعُوهُ، لَوْ كَانَتْ فَاطِمَةُ لَقَطَعْتُ يَدَهَا»

**“Hakika Bani Israel walikuwa anapoiba mtukufu miongoni mwao humsamehe, na pindi anapoiba dhaifu humkata mkono. Lau ingekuwa ni Fatima (yaani binti ya Mtume) ameiba ningemkata mkono.”**
[Sahih al-Bukhari]

Ama kuhusu usalama wa wanawake, ulimwengu wa kiliberali wa Kimagharibi hauwezi kutatua mgogoro huu mkubwa. Tunaona uhalifu wa kutisha dhidi ya wanawake unaokithiri ndani ya nchi huria za Kimagharibi na takwimu zinazofanana zina akisi ndani ya nchi hizo zinazofuata nyayo za mfumo wa Kimagharibi. Katika zama za enzi za kati, karibia kila tamaduni isipokuwa Uislamu ziliwakandamiza wanawake kwa namna tofauti na watu wa wakati huo walitambua ukandamizaji huo; hata hivyo, usekula huria na kauli mbiu zao za kuvutia, kama uhuru wa kibinafsi, usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake uliathiri usalama wa kweli na heshima kwa wanawake ndani ya jamii hizi. Lakini bado watu wanadanganyika na kauli mbiu hizi na wanashindwa kutambua athari mbaya iliyoletwa na kanuni hizi moja kwa moja. Uislamu pekee ndio unaoweza kuhakikisha usalama wa mwanamke ambao utadumisha heshima yake na kuwaadhibu wahusika wa uhalifu bila ya kulegeza msimamo maadili ya Kiislamu yaliyowekwa na Muumba wa Ulimwengu.

(وَإِذَا الْمَوْءُودَةُ سُئِلَتْ * بِأَيِّ ذَنبٍ قُتِلَتْ)

**"Na msichana aliye zikwa hai atapo ulizwa, Kwa kosa gani aliuliwa?"** [At-Takwir, Aya ya 8-9]

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut tahrir na**

**Faizul ibn Ahmed**

JIBU LA SWALI

# Namna ya Kuamiliana na Ukaaji Uchi Ulioenea



**Swali:**

Assalamu alaikum wa rahmatullahi wa barakatuhu, sheikh wetu. Namuomba Mwenyezi Mungu Akuhifadhi na Akupe afya njema kwa ajili ya hii daawa na dini na Akupe maisha marefu katika ibadah Yake na Akujaalie uishuhudie Khilafah ya pili iliyoongoka. Namuomba Mwenyezi Mungu Aihifadhi na Aipe nguvu daawah, katika kulingania maisha ya Kiislamu, na kuunganisha Ummah wetu chini ya bendera moja. Ameen

Swali langu ni kuhusu wanaume kuangalia wanawake. Katika nchi za Magharibi, wanawake wengi hudhihirisha uchi (nywele na mikono kwa uchache - na karibia kila kitu majira ya joto). Mimi nafahamu kwamba kuona awrah (uchi) zao ni haram kwa wanaume, iwe ni wanawake wanaovutia au la, kama vile ilivyo haram kwa mwanamume kuona uchi wa mwanamume mwenziwe pamoja na kuwa hawavutiani.

Nafahamu kwamba "jicho la kwanza" halina makosa, na kuangalia tena baada ya hapo kwa hali yoyote ni haram. Katika maisha ya kila siku katika nchi za Magharibi, mwanamume hukutana na wanawake wanaodhihirisha awrah kila siku. Katika hali kama kuendesha gari au kutembea, huweza mtu akaangalia mara moja tu, lakini, hili kulitekeleza kazini, shule na madukani ni jambo lisilowezekana kutekelezwa.

Ni jambo lisilowezekana kabisa kwa mwanamume kuingililiana na wafanyakazi wenzake wa jinsia ya kike bila kuwaona awrah. Lau atamuona awrah yake kwa mara ya kwanza, basi kwa mara nyengine yoyote atakayokutana naye, itambidi afunge macho yake au aangalie sakafu/chini. Hapa simaanishi kumuangalia na matamanio kivyovyote. Huenda hata mwanamke mwenyewe sio wa kuvutia, lakini kwa maingiliano, mwanamume yambidi kumuangalia awrah yake - lakini ameruhusiwa tu jicho la kwanza (kama ninavyofahamu)

Mwanafunzi wa Kiislamu hatoweza kushiriki katika masomo darasa ambalo mwalimu ni mwanamke ambaye anadhihirisha awrah yake. Baada ya kumuangalia mwanzo wa masomo, basi itakuwa haram kwake kumuangalia tena mpaka mwisho wa masomo, hata kama ni mzee au havutii. Kwani anadhihirisha awrah, ambayo ni haram kuangalia.

Hali hii inafanana na madukani vilevile.

Mwanamume hatoweza kuingililiana na mwanamke ila kwa kuangalia chini au kufunga macho yake. Hata kama havutii, haruhusiwi kumuangalia awrah yake.

**Swali langu:**

Je dhana yangu iko sawa - kuwa kumuangalia mwanamke wa kando (ajnabiya) ni haramu ila kwa jicho

*Endelea... UK 11*


Email: info@uqab.or.ke

la kwanza, hata kama havutii, kama vile kumuangalia awrah mwanamume ni haram pamoja na kuwa hakuna kuvutiwa kwake? Kama ni haram, je kufanya kazi ambayo ndani yake kuna kuingililiana na wanawake ambao hudhirisha awrah zao yaruhusiwa juu ya msingi wa kila jambo kwa hukmu yake, kwa msingi wa dharurah?

Naomba ueleze haswa kinachomaanishwa na "jicho la kwanza"?

Naomba pia ueleze maana haswa ya wanateremsha macho yao "Yaghuddhoo Absarihin/Absarihim" na hutekelezwa wakati gani?

Mwenyezi Mungu Awajazi kheri ewe Sheikh

Kutoka kwa: Saifudeen Abdullah) Mwisho

**Jibu:**

Waalaykum Salam Warahmatullahi Wabarakaatuh,

Kuhusu ukaaji uchi ulioenea ambapo ni vigumu kujikinga nako katika dhuruf ya Dola zilizopo sasa ambazo hazitabikishi Uislamu, kulingana na hali hizi Mwenyezi Mungu ametuamrisha mambo mawili:

**Kwanza:** Kufumba jicho, yaani tuinamishe macho kwa kiwango cha kuweza kutembea na kutekeleza kazi...

**Pili:** Tusifuatilize mtazamo wa ghafla kwa mtamazamo mwengine...

Na tumeyafafanua hayo katika kitabu cha Nidhamu ya Kijamii kuhusu jibu la swali lako tukasema:

(...Tangu tulipovamiwa na hadhara ya Kimagharibi, Na kutawala Miji ya Waislamu kwa nidhamu za kikafiri wanawake wasiokuwa wa Kiislamu wamekuwa wakitoka nje nusu uchi: Wanadhihirisha vifua vyao na migongo yao, Nywele na mikono na miundi. Wakawa baadhi ya wanawake Waislamu wanawaiga nao wanatoka kwenda masokoni kwa sura hii, mpaka ikawa mtu hawezi kutofautisha wanapokwenda sokoni baina ya mwanamke wa Kiislamu na asiyekuwa Muislamu, au akiwa amesimama Dukani anataradhia bei. Na wanaume Waislamu ambao wanaishi katika hii miji hawawezi wao peke yao kuondoa munkar hivi sasa, na hawawezi kuishi katika miji hii pasi na kuona hizi nyuchi. Kwa kuwa maumbile ya kimaisha ambayo wanaishi, na sampuli ya nyumba wanazoishi, yalazimisha mwanamume kuona uchi wa mwanamke, na mwanamume yeyote hawezi kujilinda asione nyuchi za wanawake, mikono yao, vifua vyao na migongo yao, miundi yao na nywele zao, namna atakavyojaribu asione, isipokuwa anapokaa nyumbani kwake na asitoke nje, na hili haliwezekani kabisa, kwani yeye anahitaji kuwa na mahusiano na watu katika kuuza na kununua, kuajiri na kufanya kazi, na mengineo ambayo ni katika dharura ya kimaisha. Na hawezi kuyafanya hayo huku akichunga asione hizi nyuchi. Na uharamu wa kuangalia uchi uko wazi katika Kitabu na Sunnah je afanye nini? Kutoka katika hili tatizo inakuwa katika sehemu mbili:

Kwanza, ni kuangalia kighafla bila kukusudia kile anachokishuhudia njiani na hili husamehewa mtazamo wa kwanza na ni juu yake asirudie mara ya pili, Kutokana na kile alichopokea Jarir bin Abdillah asema:

«سَأَلْتُ رَسُولَ اللَّهِ ﷺ عَنْ نَظْرَةِ الْفُجَاءَةِ فَأَمَرَنِي أَنْ أَصْرِفَ بَصَرِي»

**"Nilimuiza Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) kuhusu kuangalia ghafla akaniamrisha niangalie kando"** [Amepokea Muslim]. Na kutoka kwa Ali radhi za Allah zimwendee asema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) aliniambia:

«لَا تُتْبِعِ النَّظْرَةَ النَّظْرَةَ، فَإِنَّمَا لَكَ الْأُولَى، وَلَيْسَتْ لَكَ الْآخِرَةُ»

**"Usifuatilize mtazamo wa kwanza kwa mtazamo mwengine kwani jicho la kwanza ni halali, na la pili sio halali kwako"** [Ameipokea Ahmad kutoka katika njia ya Buraydah].

Ama hali ya pili ambayo ni kuongea na mwanamke ambaye ameweka wazi kichwa chake na mikono yake na yale ambayo amazoea kifichua, basi huyu ni wajib kuangalia kando, na kufumba jicho lisimuangalie, kwa kile alichopokea al-Bukhari kutoka kwa Abdillah bin Abbas radhi za Mwenyezi Mungu ziwaendee asema:

«كَانَ الْفَضْلُ رَدِيفَ النَّبِيِّ ﷺ فَجَاءَتْ امْرَأَةٌ مِنْ خَثْعَمَ فَجَعَلَ الْفَضْلُ يَنْظُرُ إِلَيْهَا وَتَنْظُرُ إِلَيْهِ فَجَعَلَ النَّبِيُّ ﷺ يَصْرِفُ وَجْهَ الْفَضْلِ إِلَى الشِّقِّ الْآخَرِ»

**"Al-Fadhlu alikuwa akimuandama Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akaja mwanamke kutoka Khatha'm (kuuliza hukmu fulani), ikawa Al-Fadhlu anamuangalia yule mwanamke na mwanamke anamuangalia. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akawa anaugeuza uso wa Al-Fadhlu upande mwengine".** Na akasema Mwenyezi Mungu (swt):

(قُل لِّلْمُؤْمِنِينَ يَغُضُّوا۟ مِنْ أَبْصَـٰرِهِمْ وَيَحْفَظُوا۟ فُرُوجَهُمْ)

**"Waambie Waumini wanaume wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao."** [An-Nur: 30]

Na maana ya kufumba jicho ni kuinamisha. Kwa hiyo kutatua hili tatizo ni kuinamisha macho upande wa Mwanamume, pamoja na kuendelea na kazi yake ya dharura anayoifanya pamoja na mwanamke kama yule, au kupanda gari, au kukaa ukumbini kwa sababu ya joto kali, au mfano wake. Hizi haja ni katika dharura jumla za kimaisha kwa Mwanamume, Hawezi kuzikimbia wala hana uwezo wa kuzuia huu mtihani wa kufichua uchi,

*Endelea... UK 12*

basi ni juu yake kuinamisha macho kwa kulifanyia kazi andiko la ayah hii, na sio halali kwake jambo lengine kabisa.

Na wala haisemwi hapa: kwamba haya ni katika mitihani ilioenea, na ni vigumu kujichunga nayo, kwa hakika qaida hii inagongana na sheria, haramu haiwezi kuwa halali kwa kuenea mitihani, na wala halali haiwezi kuwa haramu ikawa mitihani imeenea. Wala haisemwi kuwa hawa ni wanawake wa kikafiri kwa hiyo wataamiliwa miamala ya watumwa, kwamba nyuchi zao ni nyuchi za vijakazi. Haisemwi hivyo kwa kuwa Hadith iko jumla (Aam) kwa wanawake wote, na haikusema mwanamke wa Kiislamu. Mtume (saw) asema:

«إِنَّ الْجَارِيَةَ إِذَا حَاضَتْ لَمْ تَصْلُحْ أَنْ يُرَى مِنْهَا إِلَّا وَجْهُهَا وَيَدَاهَا إِلَى الْمِفْصَلِ»

**"Hakika kijakazi anapoanza kupata hedhi sio halali kuonekana isipokuwa uso wake na viganja vyake vya mkono hadi kwenye kifundo cha mkono"** Na hadith hii iko wazi katika uharamu wa kumuangalia mwanamke, awe Muislamu au asiekuwa Muislamu, na ni jumla katika hali zote. Na wala Hafanyiwi qiyas mwanamke kafiri kwa kijakazi kwa kuwa hakuna sehemu ya kufanyia qiyas...

Na ni wajibu kwa wale wanaishi katika miji, na wanalazimika kupitia maisha ya mujtamaa' au kuamiliana na wanawake makafiri wenye kufichua nyuchi zao, kwa kununua kutoka kwako, au kuzungumza nao, au kukodi kutoka kwao, au kuwaajiri, au kuwauzia, au mengineo, wainamishe macho wakati huo, na wafupishe kwa kadri ya wanachohitajia kile ambacho ni cha dharura.) **Mwisho wa Nukuu.**

Nataraji jibu hili litakuwa limetosheleza swali lako, Na Mwenyezi Mungu Ndie Mjuzi Zaidi na Mwingi wa Hekima.

**Ndugu Yenu,**

**Atwa Bin Khalil Abu Rashtah**

**9 Dhul Hijja 1442H**

**19/07/2021 M**



Email: info@uqab.or.ke